MAMBO YA UZUSHI YA MWEZI WA RAJAB.

Imeandikwa na Shekh: Muhammad Bin Swaleh Al Utheimin.

Imetafsiriwa na : Abu AbdurRahmaan Alhadhramy.

Imepitiwa na: Yunus Kanuni Ngenda.

Amesema mwanachuoni Muhammad Bin Swaleh AlUtheimin (AllaahAmrahamu):

"KILA HADITHI iliyopokewa kueleza fadhila za Swala au Swaum katika mwezi wa Rajab ni dhaifu sana!!

Bali baadhi ya wanavyuoni wamesema ni maudhui haswa yaan zimetungwa na kusingiziwa uongo Mtume (SwallaAllaahu aleihi wa sallam), kwahiyo haifai kwa mtu kutegemea hadithi hizo.

Haifai kwa yeyote kutegemea hadithi hizo, akahusisha Rajab kwa swaum au swala, kwasababu kufanya hivyo ni uzushi, na Mtume swalla LLahu aleihi wa sallam amesema:

"Kila bid'a ni upotofu na kila upotofu makazi yake motoni" !

Ama Hadithi eti Mtume (Swalla Allaahu 'aleihi wa sallam) alikuwa akisema inapoingia Rajab: "Allahumma Baarik Lanaa Fii Rajab wa Shaabaan wa ballighnaa Ramadhan..".

Lakini hadithi hii ndugu zangu nisikilizeni ninayo yasema, ni dhaifu bali ni munkar, haiswihi kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'aleihi wa sallam..)

Kwasababu hiyo, haitakikani kwa Muislamu aombe Dua hii kwasababu haikuswihi kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'aleihi wa sallam..)

Mimi nitawaambia kuwabainishia haki, kuwa mwezi wa Rajab hauna Swala maalum inayohusu mwezi huu, sio katika usiku wa Ijumaa ya kwanza wala hamna Swaum inayohusu mwanzo wa mwezi wala siku yoyote ile...

Wala haijuzu kwa mtu yeyote kuhusisha wakati maalum au sehem maalum kwa ajili ya ibada, wakati Allaah na Mtume wake hawajaamrisha hilo...

Sababu sisi tumeamrishwa kumuabudu Allaah kulingana na sheria yake wala sio matamanio yetu wala hisia zetu..

Uwajibu juu yetu ni kusema: Tumesikia na kutwii, Tufanye alichoamrisha Allaah na kujiepusha na alichokikataza Allaah, wala sio kujiwekea sheria kwa binafsi yetu na ibada ambazo Allaah hakuziamrisha wala Mtume wake (s.a.w)...

Enyi Waislamu! Hakika katika yale yaliyokuja katika kitabu cha Allaah, na yale yaliyothibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaah 'aleihi wa sallam), katika 'amali njema yanatosheleza kutokana na hadithi dhaifu ama feki za uongo, na lau kama binadamu atamuabudu Allaah kwa yale yaliyothibiti peke yake, Yatosheleza kuwa amemuabudu Allaah kwa elimu, akitarajia malipo kutoka kwa Allaah na kuiogopa adhabu Yake"...

TNB: Nasema: "Elewa kuwa kila hadithi iliyokuja kutaja fadhila za Rajab... basi haikuthibiti kama walivyoeleza maulamaa... chunga muislam usije ukaangukia katika uzushi".

Chanzo:

http://www.ibnothaimeen.com/all/khotab/article_468.shtml

http://3bbr.com/bb/rgb/rgbm.mp3.